JARIDA
SEKRETARIETI YA AJIRA

Toleo namba 1, Januari 2024

*Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma*

# Rais Samia aendelea kushusha neema ya Ajira kwa vijana



## HABARI KUU

1. Rais Samia aendelea kushusha neema ya ajira kwa vijana
2. Kikwete aipongeza Sekretarieti ya Ajira
3. Mfumo mpya wa usaili kielektroniki kuzinduliwa
4. Waajiriwa wapya wa Sekretarieti ya Ajira watakiwa kuzingatia maadili
5. Sekretarieti ya Ajira yatoa elimu kupitia vyombo vya habari

## Kikwete aipongeza Sekretarieti ya Ajira




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete*

Kikwete alitoa pongezi hizo wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika mjini Morogoro

*...uk 4*

## 'Watanzania changamkieni fursa za kazi Serikalini'- Bomani



*Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani*

"Niwahakikishie Watanzania wote kuwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma tunazingatia sheria na taratibu zote"

*... uk5*

Sekretarieti ya Ajira
Sekretarieti_ya_Ajira
Ajirapsrs
AjiraTV
Mawasiliano 0262160350 www.ajira.go.tz

# Rais Samia azidi kushusha neema ya ajira kwa vijana

Jina la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan limeendelea kung'ara kwenye kila pembe ndani na hata katika uga wa kimataifa.

Ukiachilia mbali dhamira yake ya kuhakikisha Tanzania inakuwa ni rafiki kwa mataifa mengine kwa kukuza diplomasia ya uchumi hapa nchini, vile vile Rais Dkt.Samia ameendelea kuitekeleza kwa vitendo dhana ya maendeleo ya vitu na maendeleo ya watu.

Kwa namna yoyote utakayoamua kutazama bila shaka macho yako hayataacha kuona namna Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyozidi kuwaneemesha Watanzania katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na ongezeko la vibali vya ajira kwa sekta tofauti.

Tangu ameingia madarakani Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan amehakikisha anaboresha zaidi maisha ya wananchi wa kawaida pamoja na maslahi kwa watumishi wa umma na pia kuendelea kuwa shujaa na mkombozi wa wengi kwa kutoa nafasi nyingi za ajira za umma na vilevile kutengeneza mazingira wezeshi kwa sekta binafsi ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia kutoa ajira hususani kwa vijana.

Katika kulitekeleza hilo, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kama chombo chenye dhamana ya kusimamia mchakato wa ajira katika utumishi wa umma imeendelea kuhakikisha inatekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia haki,usawa na uwazi.



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan***

Aidha,kwa kipindi cha kuanzia (Julai-Disemba 2023) Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma imefanikisha mchakato wa ajira katika taasisi mbalimbali ambapo wasailiwa 5,257 walipangiwa vituo vya kazi kutokana na usaili uliofanyika katika kanda nne ambazo ni Dar es salaam, Mwanza, Mbeya na kituo maalum kimoja cha Zanzibar.

Katika idadi hiyo ya waliopangiwa vituo vya kazi, wanawake ni 1,911 na wanaume ni 3,346 ambao wameenda kulitumikia Taifa katika maeneo mbalimbali.

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba saili tano zilifanyika na waombaji wa kazi 55, 603 walituma maombi yao na kati ya hao waombaji 33,786 waliitwa kwenye usaili.

***Inaendelea uk; 3***



***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan***

# Rais Samia azidi kushusha neema ya ajira kwa vijana




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan*

Usaili huo ulihusisha waajiri mbalimbali ikiweno Wizara za serikali, Idara zinazojitegemea, Wakala wa serikali, na Mamlaka za serikali.

Waajiri wengine ni hospitali za kikanda taasisi za elimu na vyuo vikuu pamoja na vyuo vya kati, Mabaraza ya serikali tume za serikali, mashirika ya umma, sekretarieti za mikoa, Mamlaka za serikali za mitaa pamoja na Bodi za serikali.

Kwa ujumla, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan ameendelea kutoa vibali vya ajira kwa kasi kubwa huku Sekretarieti ya Ajira ikiendelea kuhakikisha ajira hizo zinawafikia wananchi na kuendesha mchakato wa ajira kwa ushindani.





*Wasailiwa mbalimbali wakiwa kwenye Usaili wa kuandika (mchujo) ili kupata wataalamu mbalimbali wa kujaza nafasi za kazi katika Serikalini.*

## Mhe. Simbachawene awataka waajiri kuimarisha usawa na kuondoa ubaguzi mahali pa kazi




***Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene***

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene ametoa rai kwa Waajiri wote katika taasisi za umma kusoma, kuelewa na kutumia kikamilifu Mwongozo wa Ujumuishwaji wa Jinsia na kuzingatia masuala ya Jinsia katika utekelezaji wa majukumu yao.

Amesema hayo wakati wa tukio la uzinduzi wa Mwongozo wa Ujumuishwaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma na Ufunguzi wa Mafunzo ya Wanawake Awamu ya Tatu na Nne yaliyoendeshwa na Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Serikali ya Finland tarehe 16 Oktoba, 2023 katika ukumbi wa Hoteli ya Hyatt Regency Jijini Dar es salaam.

Mhe. Simbachawene ameilekeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kusambaza mwongozo huo kwenye mamlaka zote za ajira katika Utumishi wa Umma na kushirikiana na Mamlaka hizo kuendesha mafunzo ili kuimarisha usawa na hatimaye kuondoa aina zote za ubaguzi mahali pa kazi.

"Ninawaelekeza waajiri wote katika taasisi za umma kuandaa Mpango kazi wa namna ya kutekeleza afua za usimamizi wa masuala ya jinsia mahala pa kazi na kutenga bajeti kwa kila mwaka wa fedha ili kumuwezesha Mratibu wa masuala ya Jinsia wa Taasisi husika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na uratibu wa mafunzo ya Jinsia katika Utumishi wa Umma kwenye Taasisi husika" alisisitiza Mhe. Simbachawene.

Vilevile, amemuelekeza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-UTUMISHI kushirikiana na Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuzifikia Mamlaka zote za Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 ili kutoa mafunzo kuhusu Mwongozo huo ili kila mtumishi wa umma apate uelewa wa kutosha na kuepuka kuwa na ubaguzi mahali pa kazi.

Vile vile, Mhe. Simbachawene amefafanua kuwa ili Taifa liweze kufikia usawa wa kijinsia, hasa kwenye masuala ya uongozi, hakuna budi kushirikisha wanaume katika utekelezaji wa mipango na jitihada mbalimbali za kufanikisha azma za wanawake kuwa viongozi.

"Kila mmoja anaona kuwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kinara na mfano wa kuigwa katika kuinua wanawake na ameendelea kujipambanua katika uimarishaji wa haki na uwezeshaji wa wanawake kwa kuwateua na kuwapatia nafasi za uongozi.

Amesema amefurahi kuona wanaume pia wamealikwa kwenye kongamano hilo na baadhi ya wakufunzi kwenye programu hiyo ni wanaume. Hivyo, ameitaka Taasisi ya UONGOZI kuendelea kuwashirikisha na kuwahusisha kikamilifu wanaume kwenye programu hii ili kuleta matokeo yenye tija.

Mhe. Simbachawene alihitimisha hotuba yake kwa kutoa shukrani za dhati kwa wadau wa maendeleo wakiwemo Serikali ya Finland, Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa (UN WOMEN) kwa kuendelea kuiwezesha Taasisi ya UONGOZI kifedha na kiutaalamu (Financial and Technical Support) katika kutimiza majukumu yake kuwajengea uwezo viongozi hususan wanawake.

***inaendelea uk 5***

## Mhe. Simbachawene awataka waajiri kuimarisha usawa na kuondoa ubaguzi mahali pa kazi

***Kutoka uk 4***

Naye, Katibu Mkuu – UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi amesema Mwongozo huo unalenga kuweka mazingira bora na wezeshi ya ujumuishwaji wa jinsia katika Utumishi wa Umma ili kuongeza tija katika utendaji kazi na kuimarisha masuala ya haki na usawa kati ya Wanaume na wanawake kwa ngazi zote katika Utumishi wa Umma.

"Kupitia mwongozo huo, tunataka kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika nafasi za Uongozi na maamuzi ikiwa ni kipaumbele cha Serikali kuendeleza wanawake na kuwajengea uwezo na kujiamini katika utekelezaji wa majukumu yao" ameongeza.

Bw. Mkomi amebainisha kuwa, azma ya Serikali kupitia lengo namba tano (5) la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030 kuhusu kufikia Usawa wa Kijinsia asilimia 50 katika uongozi, hivyo pamoja na jitihada za Ujumuishwaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma ambazo zimeendelea kufanywa na Serikali, bado baadhi ya Taasisi za Umma hazijaweza kujumuisha kikamilifu masuala ya Jinsia katika mipango na bajeti za Taasisi husika.

Ameongeza kuwa, uandaaji wa Mwongozo huo umepita awamu zote muhimu na kushirikisha kikamilifu wadau mbalimbali ikiwemo Wakurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Wizara zote ambao walitoa maoni yao.



***Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwa na Naibu Katibu Mkuu Bw. Xavier Mrope Daudi***



***Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Juma Selemani Mkomi***

***"Tunataka kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika nafasi za Uongozi na maamuzi ikiwa ni kipaumbele cha Serikali kuendeleza wanawake na kuwajengea uwezo na kujiamini katika utekelezaji wa majukumu yao" Katibu Mkuu Bw. Juma Selemani Mkomi,***

# Naibu Waziri Ridhiwani Kikwete aipongeza Sekretarieti ya Ajira

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete amelipongeza Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa Umma kutokana na uendeshaji wa mchakato wa ajira unaozingatia haki jambo ambalo limepelekea kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi.

Mhe.Kikwete ameyasema hayo wakati akifungua kikao cha Baraza hilo kilichofanyika mjini Morogoro.

Aidha Mhe. Ridhiwani Kikwete amelielekeza Baraza hilo kuendelea kuboresha mfumo ili wasailiwa waanze kufanya usaili katika mikoa na wilaya wanazoishi bila ulazima wa kusafiri kwenda mikoa mingine nje ya maeneo yao hali ambayo itawapunguzia gharama za usafiri, malazi na hasa ikizingatiwa wasailiwa wengi wanatoka kwenye familia zenye kipato cha chini.

Akitoa ripoti kwa kikao hicho mbele ya Naibu Waziri, Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani alibainisha baadhi ya changamoto zinazoikabili taasisi na kueleza namna taasisi hiyo imekuwa ikikabiliana nazo.

Miongoni mwa changamoto hizo ni uwepo wa baadhi ya miundo ya utumishi ambayo haiendani na wakati na kusababisha malalamiko kutoka kwa wadau waliojipatia sifa za kitaalamu na kitaaluma ambazo hazijatajwa na miundo ya utumishi wa umma.




***Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwenye kikao kilichofanyika Desemba 20 mwaka 2023 mjini Morogoro.***



***Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani (aliyesimama) akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa ofisi hiyo Mkoani Morogoro.***

“Baadhi ya waajiri huchelewesha mchakato kwa kutotoa ushirikiano stahiki pale hoja zao zinapokinzana na sheria zilizopo.” Alisema Bomani. Akijibu baadhi ya changamoto hizo

Naibu Waziri Ridhwani Kikwete alisema suala la miundo linafanyiwa kazi pia ameagiza Waajiri nchini kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma na kutoa ushirikiano kwa Sekretarieti ya Ajira pale unapohitajika.

Aidha, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma huendesha usaili kwa mujibu wa sheria na kuzingatia taratibu na kanuni zilizowekwa ikiwemo ushindani, haki na usawa.

# Matukio katika Picha; Kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete*




*Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (aliyekaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.*





*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete na Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira Bw. Innocent Bomani (waliokaa katikati) wakiwa na viongozi wa Idara, vitengo na baadhi ya wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wa Sekretarieti ya Ajira.*

# ‘Watanzania changamkieni fursa za kazi Serikalini’ -Bomani

Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani amewataka Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali za ajira zinazotangazwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa umma.

Bw. Bomani ametoa wito huo hivi karibuni wakati akizungumza na baadhi ya wasailiwa Jijini Dodoma na kusisitiza kuwa waombaji wa kazi hawapaswi kukatishwa tamaa na maneno ya watu.

“Mitaani kuna maneno mengi sana ambayo watu wanajaribu kuyazungumza kuhusu mchakato wa ajira katika utumishi wa umma, lakini niwahakikishie Watanzania wote kuwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma tunazingatia sheria na taratibu zote” alisema Bomani.

Aidha, Kaimu Katibu huyo amesisitiza kuwa mchakato wa ajira unaendeshwa kwa haki na ushindani na kuwataka waombaji kazi kuwa na maandalizi mazuri wanapoitwa kwenye usaili.

“Niwasisitize Watanzania kuchangamkia fursa mbalimbali za ajira zinazotangazwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na kuna watu wengi wanaoweza kuwa na ushuhuda wa namna walivyopitia mchakato wote wa ajira na hatimaye kupangiwa vituo vya kazi bila upendeleo” aliongeza Bomani.



***Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani.***

Katika hatua nyingine, Kaimu Katibu huyo amewataka waombaji kazi kuhakikisha wanazingatia maelekezo yanayotolewa kwenye matangazo ya kazi wanazoziomba ili kuepuka usumbufu na kusababisha kukosa fursa nyingi na pia amewakumbusha wawe na taarifa sahihi kuhusu mchakato wa ajira ili kuepuka utapeli unaofanywa na baadhi ya watu wasio na nia njema.

“Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma tuna vyanzo vyetu rasmi vya kutoa taarifa ikiwemo tovuti na mitandao ya kijamii na pia tunatumia vyombo vingine vya habari kutoa taarifa zetu, hivyo wanaotafuta nafasi za kazi lazima wawe makini wanapotafuta taarifa sahihi za kazi”, alisema Bomani.

Aidha,kiongozi huyo ameweka wazi kuwa ofisi hiyo imeendelea kufanyia kazi maoni mbalimbali kutoka kwa wadau yenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa taasisi hiyo na kuleta matokeo chanya kwa wananchi.

“Tunaendelea kufanya maboresho makubwa yenye lengo la kuwa na mifumo bora zaidi na kuhakikisha tunaufanya mchakato wa ajira kuwa rafiki kwa Watanzania wote” aliongeza.

“Tunakuja na mfumo mzuri wa kufanya usaili wa mchujo (kuandika) kwa waombaji wa kazi ambao utaondoa changamoto nyingi ambazo zimekuwa zikielezwa na watu wengi ikiwemo suala la kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya usaili” aliongeza.

Kwa mujibu wa Bw.Bomani, wataalamu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wanaendelea kuboresha mifumo inayotumiwa na ofisi hiyo ili kuufanya mchakato wa ajira kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia.

# Mfumo mpya wa usaili wa kielektroniki kuzinduliwa

Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inatarajia kuzindua mfumo mpya wa usaili wa mchujo (kuandika) ambao utaondoa adha kwa wasailiwa kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Akifafanua kuhusu mfumo huo Mkuu wa Idara ya TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika utumishi wa umma Bw. Samwel Tanguye amebainisha kuwa mfumo huo wa kupima uelewa na ufahamu wa wasailiwa (Online aptitude test system) utaondoa changamoto nyingi wanazokumbana nazo wasailiwa katika mchakato wa kutafuta ajira serikalini.

"Tumejenga mfumo ambao utawawezesha vijana kufanya usaili wa kuandika kwenye vituo maalumu katika maeneo jirani na wanakoishi" alisema Bw.Tanguye

Aidha, Mkuu huyo wa Idara ya TEHAMA amebainisha kuwa mfumo huo uko tayari na unatarajiwa kuanza kutumika hivi karibuni

"Mfumo huo ambao umekamilika utaanza kutumika hivi karibuni na utawawezesha vijana kukwepa zile gharama zilizokuwepo awali kwa hiyo hawatalazimika kusafiri kwenda mbali kwa ajili ya kufanya usaili ule wa kuandika (mchujo)" aliongeza.

Katika hatua nyingine Bw.Tanguye ameeleza kuwa kupitia mfumo huo mpya usaili wa mchujo utafanyika kwenye vituo vyenye kompyuta zenye mtandao wa intaneti katika wilaya na mikoa wanakoishi wasailiwa hao.



*Mkuu wa Idara ya TEHAMA, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Mhandisi Samwel Tanguye*

"Kwa hiyo hii ni faraja kwa vijana wengi wanaotafuta kazi ambao walikuwa wanatamani muda mrefu na kupitia mfumo huu tumeweza kujibu na kuwaondolea changamoto walizokuwa wanakutana nazo hapo awali".

Katika kuhakikisha ubora na ufanisi wa mfumo huo Mkuu huyo wa Idara ya TEHAMA amebainisha kuwa wajumbe wa Sekretarieti ya Ajira wamepata nafasi ya kuupitia na kuona namna utakavyokuwa ukifanya kazi.

"Kazi ya leo ilikuwa ni kuwapitisha wajumbe wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ili waweze kuuona na tupokee maoni yao na baada ya kazi hii tutawaita wadau wengine wakiwemo wasailiwa waje na wao wajaribu kufanya usaili kwa njia ya kidigitali na tuweze kupata maoni yao kabla hatujaanza kuutumia mfumo wetu rasmi" alisema


***Inaendelea uk 10***



***Viongozi wa Idara na vitengo, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wakiupitia mfumo mpya wa usaili wa mchujo unaotarajiwa kuzinduliwa, mfumo huo wa kielektroniki utawawawezesha wasailiwa kufanya usaili kwenye maeneo yao bila kulazimika kusafiri kwenda sehemu zingine kama ilivyokuwa awali.***



***Wajumbe wa Sekretarieti ya Ajira wakiupitia mfumo mpya wa Usaili wa Mchujo na kutoa mapendekezo yao kabla ya mfumo huo wa kielektroniki kuzinduliwa***





***Watumishi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Idara ya TEHAMA wakiupitia mfumo mpya wa Usaili na kuufanyia maboresho***

***kutoka uk 9***

katika Utumishi wa Umma Bi. Sophia Kaduma amesema kuwa mfumo huo ni mzuri na utaondoa changamoto nyingi kwenye mchakato wa ajira

“Huu mfumo utatusaidia kupunguza muda tunaotumia na utafanya ajira za watumishi wa serikali kuchakatwa kwa muda mfupi na pili mfumo huu utasaidia watu kutokukutana na kupunguza vishawishi”

Mwenyekiti huyo ameongeza kuwa hatua hiyo itawawezesha wasailiwa kujibu maswali kwa njia ya mfumo na kusisitiza kuwa jambo hilo litaongeza ushindani kwa watu wanaotafuta ajira na pia kuboresha zaidi mazingira ya utendaji haki na usawa kwa kila mtu.

“Upendeleo haupo kwa sababu tunachofanya Sekretarieti ya Ajira ni kushindanisha watu kuona uwezo wao na yule anayekuwa na uwezo anapata lakini kwenye mfumo ndio inaimarishwa zaidi na kuonesha kuwa kila mtu ana nafasi, mtoto wa masikini na mtoto wa mtu mkubwa wote wana nafasi kupitia sekretarieti ya Ajira kwa hiyo ni mfumo shindani ili kuibua ujuzi tunaouhitaji” alisisitiza Bi.Kaduma.

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imekuwa ikisikiliza maoni ya wadau na kuyafanyia kazi hivyo mfumo huo mpya utakuwa suluhisho kubwa kwa watu wengi wanaotafuta ajira ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamika kuhusu gharama kubwa wanazotumia kusafiri kutoka maeneo mbalimmbali kwa ajili ya kufanya usaili wa kuandika (mchujo).

# Viongozi wa Sekretarieti ya Ajira wakutana kujadili mfumo mpya wa Usaili





*Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bi. Sophia Kaduma akiwa na Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani katika kikao cha kupitia mfumo mpya wa usaili wa kuandika (mchujo) unaotarajiwa kuzinduliwa utakaowawezesha wasailiwa kufanyia usaili katika maeneo yao husika wanapoishi.*



*Kutoka kushoto Makamu Mwenyekiti wa Sekretarieti ya Ajira Kamishna Said Kamugisha, Jaji Clecencia Makulwa (Mjumbe) Bi Bernadetha Ndunguru (Mjumbe) na Bi Riziki Kuhanwa (Mjumbe)*





*Kutoka kushoto Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Bi Neema Kivugo, Mkuu wa Idara ya Tehama Mhandisi Samwel Tanguye, Mkuu wa Idara ya Udhibiti wa Ubora Bw. Bazil Koni, na Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Tathmini, na Ufuatiliaji Bw. Joachim Nyanda.*

# RC Mtaka aipongeza Sekretarieti ya Ajira



*Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mh. Anthony Mtaka*

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mh. Anthony Mtaka ameipongeza Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa kufanya kazi zake kwa weledi bila upendeleo.

Mh. Mtaka alitoa pongezi hizo alipotembelea banda la Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wakati wa maonesho ya kilimo (Nanenane ) Jijini Mbeya.

Mkuu huyo wa Mkoa alibainisha kwamba Sekretarieti ya ajira imekuwa ikifanya Shughuli zake kwa haki bila upendeleo pamoja na kuzingatia sheria huku akiipongeza taasisi hiyo kwa kusikiliza maoni ya wadau na kuyafanyia kazi.

"Miaka michache ya nyuma watu walipokuwa wakiomba kazi kulikuwa na baadhi ya vyuo vilikuwa vina malalamiko kwamba mtu akiomba kazi kwa watu ambao walisoma ngazi ya diploma na cheti katika vyuo vikuu ambavyo havijasajiliwa na NACTE walikuwa wanapata changamoto, lakini pia kwa kuwa Sekretarieti inasikiliza malalamiko na maoni na watu walipoleta hizo hoja zilifanyiwa kazi na watu hao wakaitwa kwenye usaili" alisema.

Aidha, Mhe. Mtaka alisema kuwa kupitia mifumo imara iliyowekwa na Sekretarieti ya ajira wananchi wengi wamekuwa na imani na kazi inayofanyika.

"Tunawashukuru sana Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Sekretarieti ya Ajira kwa sababu tunao vijana wa Kitanzania ambao mara ya kwanza walikosa nafasi kwenye usaili ulioendeshwa na Sekretarieti ya ajira lakini baadae walipigiwa simu kuitwa kwenye ajira kutoka kwenye orodha ya kanzidata na hao walioitwa ni watu wa kawaida ambao sio watoto wa viongozi hivyo watu wengi wanaona mchakato ulivyo na usawa kwa kuwa mtu anakwenda anafanya usaili na anajipima mwenyewe na kule kwenye malalamiko Sekretarieti imechukua hatua"aliongeza Mh. Mtaka.

Kadhalika, Mhe. Mtaka aliongeza kuwa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kazi kubwa kwenye kutangaza nafasi mbalimbali za ajira kwa makundi yote.

"Tunamshukuru sana Mh. Rais kwa sababu kwenye kipindi chake cha miaka miwili tumepata ajira nyingi za makundi mengi ikiwemo vyombo vya dola, sekta ya elimu, sekta ya afya na makundi mengine mengi na utaona taasisi mbalimbali za Serikali zinatangaza ajira kwenye aina tofauti za utaalamu hili ni jambo kubwa sana la kuipongeza Serikali"

"Kwa mfano, tulipopata changamoto kwenye miradi mbalimbali ya halmashauri hususani madarasa na vituo vya afya, ilionekana kwamba kuna changamoto ya wahandisi kwa hiyo Serikali ikatangaza nafasi nyingi za kazi kwa wahandisi kwenye halmashauri zote pamoja na sekretarieti za mikoa" aliongeza Mh. Mtaka.

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa Mkoa wa Njombe amewataka waombaji wa kazi kutokata tamaa pale wanaposhindwa kupata kazi na kuwasisitiza kujaribu mara kwa mara na kuondoa dhana ya kuwepo upendeleo.

## Sekretarieti ya Ajira yashiriki kutoa elimu kwa umma kwenye maonesho ya Nanenane jijini Mbeya




*Kaimu Mkuu wa Idara ya Ajira Somwana Manjenga (Wa kwanza kulia) na Afisa Utumishi Mwandamizi Kissa Kasebele wa PSRS wakizungumza na moja ya wadau waliotembelea banda la Sekretarieti ya Ajira kujifunza taasisi hiyo inavyoendesha mchakato wa Ajira.*






*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano PSRS Bi. Lynn Chawala akisikiliza na kujibu maswali kutoka kwa waombaji kazi waliotembelea banda la Sekretarieti ya Ajira kwenye Maonesho ya Nanenane jijini Mbeya*



*Afisa Habari Beatrice Kimwaga akiwafundisha waomba kazi namna ya kuingia kwenye mfumo wa Ajira Portal*



*Afisa TEHAMA- Mhandisi Hemed Mkomwa akitoa maelezo kwa waombaji wa kazi juu ya mchakato wa Ajira unavyoendeshwa*



## Shuhuda za waajiriwa wapya waliopata ajira kupitia Sekretarieti ya Ajira

*“Nimepangiwa kituo cha Uyole, mimi sikumfahamu mtu katika mchakato wa ajira nilifata tu michakato yote ya kuomba katika tovuti (portal.ajira.go.tz/) nikaitwa katika usaili uliofanyika Dodoma na tukafanya mtihani wa kuandika nikafaulu, halafu tukafanya mtihani wa mahojiano Mungu akanisaidia nikapata kazi bila kuwa na mtu ninaemfahamu”.*
*“Joseph Nakomora Josep, muajiriwa mpya wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania(TARI)*



*Joseph Nakomora Joseph*
*Mwajiriwa Mpya*

*“Kwa kweli nawapongeza sana Sekretarieti ya Ajira na pia nawashauri vijana wenzangu ambao wamemaliza vyuo lakini wanaogopa kutuma maombi ya ajira wakati nafasi za kazi zinapotangazwa mimi nawapa ushuhuda na kuwaasa kwamba Sekretarieti ya Ajira tangu imeanzishwa imesaidia sana vijana ambao tulikuwa tunaogopa na kuamini kuwa ajira hizi zilikuwa ni kwa ajili ya watu ambao wameandaliwa jambo ambalo si kweli”*
*“Deogratius Dominick Peter muajiriwa mpya wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),*



*Deogratius Dominick Peter*
*Mwajiriwa Mpya*

*“Nilipata ajira kupitia Sekretarieti ya Ajira, pamoja na kwamba kumekuwa na dhana nyingi mtaani ambao wengi wanaamini ili upate ajira ni lazima uwe na mtu unayemjua kwenye Sekretarieti, mimi niwatoe hofu vijana wenzangu ambao wamehitimu katika vyuo mbalimbali usaili unaoendeshwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma hauna upendeleo wowote hivyo watu wanapaswa kujiandaa”.*
*“Mkufunzi wa chuo cha Ardhi Morogoro Cuthbert Ernest Kayumbo,*



*Cuthbert Ernest Kayumbo,*
*Mwajiriwa Mpya*

# Watumishi Sekretarieti ya Ajira watakiwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma

Watumishi wapya wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wametakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma katika utendaji wao.

Wito huo ulitolewa na aliyekuwa Mhasibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Christopher Nkupama (CPA) wakati akifungua mafunzo ya awali Kwa watumishi wapya kwa niaba ya Kaimu Katibu wa Ofisi hiyo mwezi Agosti mwaka 2023.

"Ndugu washiriki, mkiwa watumishi wa umma mara zote mnapaswa kujua na kuzingatia sheria na kanuni mbalimbali za utumishi wa umma" alisema Nkupama.

Aidha, katika ufunguzi huo, Mhasibu Nkupama ameeleza kuwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ina matarajio makubwa kwa watumishi hao katika kuhakikisha wanaongeza ufanisi wa kiutendaji.

"Tuna matarajio kuwa mtakapofahamu sheria na taratibu mtaongeza ufanisi katika utendaji na uwajibikaji utakuwa mkubwa, kwa kuwa sisi tunawajibika Kwa wananchi na wadau wetu wengine basi mafunzo haya yakatuongezee kitu katika kuwasaidia wananchi" aliongeza.

Katika hatua nyingine Nkupama aliwapongeza watumishi wapya wa Ofisi hiyo na kuwasisitiza kutekeleza wajibu wao ipasavyo ili kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan kutimiza malengo ya serikali kwa kutoa huduma bora kwa wananchi.



***Aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Uhasibu na Fedha, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma CPA Christopher Nkupama***

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Chuo Cha Utumishi wa Umma, Mkurugenzi wa Chuo hicho kutoka Singida Dkt.Hamis Amani ameupongeza uongozi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa kuandaa mafunzo hayo kwa watumishi wapya wa ofisi hiyo.

"Nawapongeza kwa kuandaa mafunzo haya ambayo yatawafanya washiriki wawe na uelewa wa kina kuhusu utumishi wa umma na kutambua sheria na miongozo ya Utumishi wa umma" alifafanua Dkt.Amani.

Vilevile Dkt.Amani aliwataka watumishi hao kuzingatia mafunzo hayo ili kutokwamisha utendaji wa serikali na kuchelewesha huduma kwa wananchi.

Mafunzo elekezi ya awali kwa watumishi wapya wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma yalifanyika Kwa siku tatu kuanzia Agosti 28 hadi Agosti 30, 2023 jijini Dodoma.



***Kutoka Kulia Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bw. Imani Kasagara akitoa neno la ukaribisho kabla ya kuanza mafunzo kwa waajiriwa wapya wa taasisi hiyo, viongozi wengine ni Aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Uhasibu na Fedha-PSRS, CPA Christopher Nkupama (Kati) na Mkurugenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Ndaki ya Singida Dk Hamis Aman.***

# Bomani awataka maofisa Utumishi wa Halmashauri kuzingatia haki, usawa na uwazi



***Kutoka kulia, Kaimu Mkuu wa Idara ya Ajira Bi. Somwana Manjenga, Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani, akifuatiwa na Mkuu wa Idara ya Udhibiti wa Ubora Bw. Bazil Koni na Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (CIA) Bw. Peter Chilumba***

Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani amefungua mafunzo ya mfumo wa 'Ajira Portal' kwa maofisa utumishi na maofisa TEHAMA kutoka katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ya Iringa, Dodoma, Mbeya, Singida, Songwe, Katavi, Lindi, Kagera, Rukwa, Njombe na Simiyu.

Mafunzo hayo ni maalum kwa ajili ya kuwajengea uwezo maofisa hao juu ya matumizi ya mfumo wa 'Ajira Portal' ambapo kuanzia Januari mwaka 2024 maombi yote ya ajira na matangazo ya ajira yatakuwa yanafanyika kupitia mfumo huo tofauti na hapo awali ambapo maombi yalikuwa yanawasilishwa kwa njia ya barua kwenye halmashauri mbalimbali.

Akifungua mafunzo hayo, Bwana Bomani amewataka watumishi hao kuzingatia sheria na kanuni za utumishi pamoja na kuzingatia haki, usawa na kutokuwa na upendeleo katika kuendesha mchakato wa ajira.

"Mkiingiza watumishi ambao kwa njia moja ama nyingine hawakufuata misingi ya wazi ya haki wakati wa mchakato wa ajira, maana yake unaileteа serikali shida kubwa.

Maofisa utumishi mkumbuke suala la kumuajiri mtumishi ni rahisi kuliko kumuondoa, kumuajiri ni njia ndefu inayohitaji weledi, uadilifu mkubwa lakini kumuondoa mtumishi ni njia ndefu na inayohitaji umakini mkubwa kwahiyo tunawaomba msimamie weledi na haki na muweze kukamilisha michakato ya ajira vizuri" alisema Bwana Bomani.

Aidha, Bwana Bomani aligusia juu ya uwepo wa baadhi ya watu kutaka kukiuka misingi mizuri iliyopo katika kuendesha mchakato wa ajira.

"Kwa sasa tumeona kuna dalili zimeanza kujitokeza za watu kuomba kazi kwenye maeneo yao na kutaka wale wanaofanya kazi kwa kujitolea ndio waajiriwe katika maeneo hayo, huko ni kuvunja misingi ambayo ilianzisha taifa hili na hilo kimsingi hatuwezi kukubali kwa sababu tutaanza kumong'onyoa sasa.

Tuliachiwa taifa letu likiwa na mshikamano sasa tunaanza kulivunja wenyewe hilo hatutakubali, sheria kanuni na taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali ipo wazi, sera zipo wazi.

Mtu aliyepo Lindi anaweza kuomba kazi halmashauri ya Musoma, na wa Musoma anaweza kuomba Tanga, wa Tanga anaweza kuomba Bukoba ilimradi anasifa hizo" aliongeza Bomani .

# Matukio katika Picha: Ufunguzi wa Mafunzo ya Ajira Portal



*Maofisa utumishi na Maofisa TEHAMA kutoka katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ya Iringa, Dodoma, Mbeya, Singida, Songwe, Katavi, Lindi, Kagera, Rukwa, Njombe na Simiyu wakifatilia mafunzo ya mfumo wa Ajira Portal Mkoani Morogoro.*



*Kaimu Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani akitoa hotuba yake kwa maofisa Utumishi na TEHAMA kuhusu umuhimu wa kutumia Ajira Portal katika Mchakato wa Ajira*



*Mhandisi Samwel Tanguye, Mkuu wa Idara ya TEHAMA, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma*









*Maofisa utumishi na Maofisa TEHAMA kutoka katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa wakifatilia mafunzo kuhusu mfumo wa Ajira Portal*

## Matangazo mbalimbali







## Dondoo Muhimu

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - Ndicho chombo pekee kwa mujibu wa sheria chenye Mamlaka ya kuajiri watu katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia SERA, SHERIA, KANUNAI, NA TARATIBU zinazohusu Ajira katika Utumishi wa Umma

Mchakato wa Ajira katika Utumishi wa Umma unazingatia sifa, taaluma, ushindani, uwazi, na usawa kwa mujibu wa SERA, SHERIA, KANUNI, NA TARATIBU zinazohusu Ajira katika Utumishi wa Umma

Sekretarieti ya Ajira huendesha saili mbalimbali ili kupata wataalamu wenye tija kulingana na nafasi za ajira zilizotangazwa

Saili za vitendo hufanyika kwa kada zenye mahitaji ya kubaini uwezo wa kutumia nyenzo mahsusi, ili kupima uwezo wa ujuzi wa utendaji kazi

Ni muhimu kupakia taarifa binafsi na za kitaaluma kwenye mfumo wa AJIRA PORTAL ili kuweza kuomba kazi pindi zitakapotangazwa.

Tembelea - www.ajira.go.tz



# Watumishi wapya Sekretarieti ya Ajira watakiwa kuwa wabunifu

Naibu Katibu, Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi. Samwel Tanguye amewataka Waajiriwa wapya wa ofisi hiyo kuwa wabunifu katika utendaji kazi ili kuongeza tija katika kuwahudumia wananchi.

Mhandisi Tanguye ametoa wito huo wakati wa kufunga mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma yaliyofanyika mwezi Agosti mwaka 2023 katika ukumbi wa Tume ya Uchaguzi Jijini Dodoma.

Aidha, Mhandisi Tanguye aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanatumia taaluma zao vizuri ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma na kuifanya ofisi hiyo kutimiza majukumu yake kwa weledi

"Wengi wenu hapa ni vijana tuna matumaini makubwa kuwa mtatumia taaluma zenu kuongeza tija, tumieni vizuri fursa hii kujifunza zaidi, pia muwe chachu ya mabadiliko makubwa katika taasisi yetu na tumieni heshima hii vizuri na hakikisheni mnazitumikia vyema nafasi zenu" alisema.

"Kila mmoja Kati yenu ana tabia zake lakini Sasa mjifunze utamaduni mpya wa utumishi wa Umma, kwa sababu kuna misingi yake na kwa kuwa mmekula viapo basi ni vyema mkaviishi viapo vyenu" aliongeza kiongozi huyo.

Akihitimisha hotuba yake Mhandisi Tanguye aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanazingatia mambo yote waliyoelekezwa katika mafunzo hayo.



*Mkuu wa Idara ya Tehama Mhandisi Samwel Tanguye (Katikati) akiwa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utawala na usimamizi wa Rasilimali watu, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (kulia) na Mkurugenzi wa mafunzo ya muda mfupi Sospeter Lameck kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Ndaki ya Singida, wakati wa mafunzo kwa waajiriwa wapya*



*Naibu Katibu Idara ya Tehama Mhandisi Samwel Tanguye akihitimisha mafunzo ya waajiriwa wapya kabla ya kuingia kazini, mafunzo hayo yalifanyika Jijini Dodoma*



*Waajiriwa wapya wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wakiwa katika mafunzo ya Utumishi yaliyoendeshwa na viongozi kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma, Ndaki ya Singida*

# Matukio katika Picha: Mafunzo ya Waajiriwa wapya wa Sekretarieti ya Ajira



***Mgeni rasmi Mkuu wa Idara ya Tehama, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Mhandisi Samwel Tanguye (aliyekaa katikati) akiambatana na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Bw. Imani Kasagara (kulia) pamoja na Mkurugenzi wa mafunzo ya muda mfupi Sospeter Lameck (kushoto) kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Ndaki ya Singida, katika picha ya pamoja na Waajiriwa wapya (waliosimama) mara baada ya kuhitimisha mafunzo .***



***Mgeni rasmi Mkuu wa Idara ya Tehama, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Mhandisi Samwel Tanguye (kushoto) akiwa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu Bw. Imani Kasagara***



***Mkurugenzi wa mafunzo ya muda mfupi Sospeter Lameck kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Ndaki ya Singida (wa kwanza kushoto) akitoa maelekezo juu ya utumishi wa Umma wakati wa mafunzo kwa waajiriwa wapya***






***Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Imani Kasagara akifafanua baadhi ya mambo wakati wa mafunzo kwa waajiriwa wapya***

# Sekretarieti ya Ajira yatoa elimu kupitia vyombo vya habari




***Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi Samwel Tanguye na Mkuu wa Idara ya Ajira Mstaafu Bw. Lucas Mrumapili wakiwa katika mahojiano kuhusu Mchakato wa Ajira kwenye kipindi cha Jambo Tanzania cha TBC 1***

Viongozi wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, wametoa elimu kwa umma juu ya mchakato wa ajira na kujibu hoja za wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari nchini.

Ziara hiyo ilifanyika katika mikoa ya Dar es salaam na Dodoma ambapo elimu kuhusu mchakato wa ajira ilitolewa.

Katika ziara hiyo Wakuu wa Idara za Tehama na Idara ya Ajira waliwasilisha mada mbalimbali pamoja na kujibu hoja za waandishi wa habari na wadau wengine ambao waliuliza kupitia vyombo hivyo.

Miongoni mwa mambo yaliyowasilishwa kupitia ziara hiyo ni pamoja na namna Sekretarieti ya Ajira inavyoendesha na kusimamia mchakato wa ajira katika utumishi wa umma na kuhakikisha upatikanaji wa watumishi wenye weledi.

Akizungumza kupitia kituo cha televisheni cha Clouds Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi Samwel Tanguye alieleza namna



***Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi Samwel Tanguye akiwa katika mahojiano kuhusu Mchakato wa Ajira kwenye kipindi cha Clouds 360***

ofisi hiyo inavyofanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na kusisitiza kuwa hakuna upendeleo wowote wakati wa mchakato wa ajira. "Mchakato wetu ni shirikishi sana kwa asilimia 95 unafanyika kwa njia ya mfumo na kila kinachofanyika ni kwa njia ya mtandao na kama unavyofahamu mifumo haiwezi ikabadilisha chochote na tunapoanza michakato yetu kuna hatua mpaka tunafikia kumpata mwajiriwa

Kwa upande wa jiji la Dodoma, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitembelea vituo viwili vya redio ambavyo ni AFM pamoja na C-FM ambapo

masuala mbalimbali juu ya mchakato wa ajira yaliwasilishwa kwa umma.

Akizungumza kupitia redio A FM ya Jijini Dodoma Afisa Utumishi Mwandamizi Bi. Kissa Kasebele aliwataka Watanzania wenye sifa za kuomba kazi serikalini kutafuta taarifa sahihi juu ya mchakato wa ajira ili kuepuka upotoshaji kutoka kwa baadhi ya watu wasio na nia njema.

Aidha, afisa utumishi huyo aliwataka vijana wanaohitimu vyuo kujisajili kwenye mfumo wa ajira (Ajira Portal) ili kuwapa urahisi wakati wa kuomba kazi.

Katika hatua nyingine Bi. Kasebele alisisitiza juu ya kutoa nafasi sawa kwa kila mtu mwenye sifa kushiriki katika mchakato wa ajira na kuwataka watu wote wanaoitwa kwenye usaili kuzingatia maelekezo yanayotolewa.

"Kumekuwa na changamoto kwa mtu ametimiza vigezo vyote na ameitwa kwenye usaili halafu hana vyeti halisi au mwingine hana kitambulisho, kwa hiyo ninawahimiza kufuata yale maelekezo yanayotolewa kwenye tangazo la kuitwa kwenye usaili na hata matangazo ya kazi" alisema afisa utumishi huyo.

Katika ziara hizo vyombo vingine vya habari vilivyotembelewa ni UTV, Channel 10, Clouds TV, TBC FM, TBC1 pamoja na ITV.

Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaendelea kutumia njia na mbinu mbalimbali kutoa elimu kwa umma kuhusu mchakato wa ajira ikiwemo kutumia vyombo vya habari, pamoja na mitandao ya kijamii.




*Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi Samwel Tanguye na Mkuu wa Idara ya Ajira mstaafu Bw. Lucas Mrumapili wakiwa katika mahojiano kuhusu Mchakato wa Ajira kwenye kipindi cha Morning Trumpet cha Azam TV*







*Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi Samwel Tanguye na Mkuu wa Idara ya Ajira mstaafu Bw. Lucas Mrumapili wakiwa katika mahojiano kuhusu Mchakato wa Ajira kupitia kipindi cha Sema cha Channel ten*

# Sekretarieti ya Ajira yatembelea Clouds TV kutoa elimu kuhusu Mchakato wa Ajira



*Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi Samwel Tanguye akizungumza kwenye mahojiano na Watangazaji Samuel Sasali na Kija Yunus kwenye kipindi cha 360 cha Clouds TV*



*Wasailiwa mbalimbali wakiwa katika usaili wa kuandika (mchujo) ambao huendeshwa na Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa umma, hii ilikuwa ni moja ya mada iliyojadiliwa katika mahojiano hayo.*





# Sekretarieti ya Ajira yatembelea TBC 1 kutoa elimu kwa Umma




*Mkuu wa Idara ya TEHAMA Mhandisi Samwel Tanguye na Mkuu wa Idara ya Ajira mstaafu Bw. Lucas Mrumapili wakiwa katika mahojiano kuhusu Mchakato wa Ajira kupitia kipindi cha Jambo Tanzania cha TBC 1*



*Mkuu wa Idara ya Tehama Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Mhandisi Samwel Tanguye*



*Mkuu wa Idara ya Ajira mstaafu kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Lucas Mrumapili akifafanua jambo kwenye mahojiano na TBC1 kuhusu Mchakato wa Ajira*




*Mkuu wa Idara ya Tehama Mhandisi Samwel Tanguye akichangia hoja kwenye mahojiano na TBC 1 kuhusu mchakato wa Ajira*



# Sekretarieti ya Ajira inavyowajali wenye mahitaji maalum

Mkuu wa Idara ya Ajira kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw.Lucas Mrumapili amesema kuwa ofisi hiyo inawapa kipaumbele watu wenye mahitaji maalumu kwenye mchakato wa ajira.

Ameyasema hayo hivi karibuni kupitia kipindi cha Jambo Tanzania kinachorushwa na TBC1 ya Jijini Dar es salaam.

Bw. Mrumapili alibainisha kuwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inazingatia haki na usawa na kuwapa kipaumbele zaidi watu wenye mahitaji maalumu wakati wa uendeshaji wa mchakato wa ajira.

"Watu wenye mahitaji maalumu tunawapa fursa ya kwanza kabisa kwenye kupata ajira, kwanza tunaangalia ule ufaulu wa ngazi ya chini kabisa kama amefaulu basi atapata ajira" alisema Bw.Mrumapili.

Aidha, Mkuu huyo wa Idara ya Ajira ameongeza kuwa kupitia mfumo wa ajira (Ajira Portal) muombaji wa kazi mwenye ulemavu ana nafasi ya kuainisha aina ya ulemavu aliyonayo ili kuwawezesha watendaji wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira kumpa kipaumbele.

"Kwenye mfumo anatakiwa yeye aoneshe ile hali yake kama ni mwenye ulemavu kuna mahali ambako anatakiwa aoneshe na mfumo unatunza ile taarifa" aliongeza.

Katika hatua nyingine Bw.Mrumapili amebainisha kuwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imekuwa ikiwapa kipaumbele wanawake katika nafasi mbalimbali za kazi zinazotangazwa.

Kuna suala la jinsia vilevile, pale ambapo wamefungana mwanamke na mwanaume hapo mwanamke atapewa nafasi na hiyo inafanyika kupitia mfumo".

Kwa kiasi kikubwa Sekretarieti ya Ajira imekuwa ikizingatia usawa kwa watu wote na kuhakikisha mchakato wa ajira unasimamiwa kwa mujibu wa sheria jambo linalopelekea kupata watumishi bora wanaoongeza chachu katika utendaji wa taasisi mbalimbali za umma.



***Mkuu wa Idara ya Ajira mstaafu katika Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw.Lucas Mrumapili akifafanua jambo***



***Mkuu wa Idara ya Ajira mstaafu kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw.Lucas Mrumapili akihojiwa na Azam TV kuhusu mchakato wa Ajira***

# Sekretarieti ya Ajira yatoa elimu kupitia vyombo vya habari



*Mkuu wa Idara ya Ajira mstaafu kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw.Lucas Mrumapili akielezea kuhusu Mchakato wa Ajira katika mahojiano na ITV*





*Mkuu wa Idara ya TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Mhandisi Samwel Tanguye akiwa katika mahojiano na TBC FM kuhusu mchakato wa ajira.*





*Afisa Utumishi Mwandamizi Bi. Kissa Kasebele akiwa katika mahojiano na kituo cha radio cha AFM Dodoma kuhusu Mchakato wa Ajira*





*Afisa Utumishi Mwandamizi Bi. Kissa Kasebele akiwa katika mahojiano na kituo cha radio cha C-FM Dodoma kuhusu Mchakato wa Ajira*